## HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2018 HADI JUNI, 2019

### 1.0 UTANGULIZI

**Ndugu Wananchi,**

Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ni miongoni mwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nane zilizopo katika Mkoa wa Tabora. Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 14,050 ambalo ni sawa na asilimia 18.8 ya eneo la Mkoa waTabora. Kiutawala Halmashauri yaWilaya ya kaliua ina jumla ya Kata 28, Vijiji 100 na Vitongoji 461. Kwa mwaka 2018 Wilaya ya kaliua inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 521,142 ambapo kati yao wanaume ni 260,160 na wanawake ni 260,982. Asilimia ya ongezeko la watuni 4.8% kwa mwaka.

**Ndugu Wananchi,**

Kila mwisho wa mwaka wa Serikali,Halmashauri hujipima ni kwa kiwango gani imeweza kuhudumia Wananchi wake kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka husika.Upimaji huu huiwezesha halmashauri kujua ni kwa kiwango gani imeweza kutoa huduma kwa wananchi kwa kipindi husika na kupanga mikakati ya kutatua changamoto zinazokuwa zimejitokeza kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma.

Kwa kuzingatia maelezo ya hapo juu, napenda nichukue fursa hii kutoa kwa ufupi taarifa ya utekelezaji wa shughuli za halmshauri kwa sekta mbalimbali za Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019.



Scanned by CamScanner

## 2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2018 HADI JUNI, 2019.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Juni, 2019, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imeweza kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

1. Ufunguzi wa shule za msingi 7 ambazo ni Kitaleni, Malanga, Songambele,Mwahalaja, Kagunga, Nhanga na Kadutu shule ya msingi. Pia, katika kuhakikisha zana za kufundishia zinapatikana mashuleni jumla ya vitabu vya kiada 89, 355 vimeletwa na serikali na kugawiwa katka shule zote za msingi.
2. Ujenzi wa vyumba 7 kupitia programu ya EQUIP-Tz katika shule za msingi za mnange-3,kagunga-2 na Nhanga-2 umekamilika. Pia,ujenzi wa vyumba 6 kupitia programu ya EP4R katika shule za msingi za mwangaza-3, Imalamihayo-3 umekamilika. Aidha ukamilishaji wa vyumba 27 kupitia programu ya EP4R katika shule za msingi za, Igwisi-2, Maboha-1, Kamsekwa-2, makubi-2, chemkeni-2, Ichemba-1, Kagera-2, Kipendamoyo-2, King'wangoko-1, Kazanaupate-2, busondi-2, mbeta-2, Bulela-2, Igagala-1, na Kashishi-2 uko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.
3. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa,ukamilishaji wa vyumba 2 na ukarabati wa vyumba 4 vya madarasa s/m Igagala kupitia ufadhili wa JTI.
4. Kupitia program ya EP4R halmashauri imeweza kujenga chumba kimoja cha darasa kanindo sekondari na Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Sekondari Igagala, ujenzi wa hosteli shule ya sekondali kazaroho na ujenzi wa maktaba ya shule ya sekondari Kazaroho. Aidha kupitia ufadhili wa Mamlaka ya Elimu Tanzania, Halmashauri imeweza kukamilisha nyumba ya walimu (six in one) shule ya sekondari kashishi.
5. Ufunguzi wa shule 5 mpya za sekondari za Silambo, Igwisi, Zugimlole, seleli na Ilege. Halmashauri itaendelea kuchangia katika kukamilisha mapungufu yaliyopo katika shule hizi ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.



Scanned by CamScanner

6. Usimamizi wa mitihani ya kumaliza elimu ya msingi na kufanikiwa kupeleka wanafunzi wote waliofaulu kidato cha kwanza ambapo jumla ya wanafunzi 4367 kati yao wavulana 2195 na wasichana 2172 wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza. Hivyo, niwaombe sana wananchi wa maeneo husika waendelee kuchangia ukamilishaji wa shule hizi na Halmashauri ya Wilaya itaendelea kuwaunga mkono ili kuendelea kupungaza msongamano wa wanafunzi katika shule za sekondari.
7. Pia, niishukuru serikali kwa programu ya Elimu bila malipo ambapo kwa mwaka 2018/19, Halmashauri imepokea jumla ya Tzs 1,193,529,788.13. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo; Tzs 747,480,741.55 kwa shule za msingi na Tzs 446,049,046.58 kwa shule za sekondari. Mhe. Magufuli Hoyee!
8. Ukamilishaji wa jengo la OPD katika Hospitali ya Wilaya umefanyika. Aidha ujenzi wa wodi ya wazazi katika hospitali ya Wilaya kwa kutumia mapato ya ndani uko hatua za mwisho kukamilika. Kwa sasa kazi zilizobaki ni ukamilishaji wa uwekaji wa vigae na upakaji wa rangi.
9. Ujenzi wa vituo vya afya 3 vya Usinge, Uyowa na mwongozo unaendelea.
10. Ufunguzi wa zahanati 4 za Kasungu, Nsimbo, Ibambo na Imalampaka ambapo zimepata usajili na zinatoa huduma. Hivyo, niwaombe sana wananchi muendelee kuchangia ujenzi wa miundo mbinu mingine ili kuboresha huduma za afya kwa jamii.
11. Ujenzi wa chumba cha upasuaji kituo cha Afya Kaliua kupitia mapato ya ndani ambapo kwa sasa kinatoa huduma ya upasuaji. Ukamilikaji wa chumba hiki umeboresha huduma ya mama na mtoto kwa kupunguza vifo vinavyotokanana na uzazi pingamizi ambapo takribani wastani wa wagojwa 8 wanahudumiwa kwa wiki.
12. Ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika kituo cha Afya Ulyankulu umekamilika ( Ujenzi wa wodi ya wazazi, Nyumba ya mtumishi, chumba cha upasuaji, Maabara na chumba cha kuhifadhia maiti). Hii yote ni kuboresha upatikanaji wa huduma ya Afya kwa wananchi.



Scanned by CamScanner

13. Katika kuhakikisha wazee wanapata huduma ya matibabu bure, Halmashauri imechapishwa vitambulisho 6,200 vya kuwatambulisha wazee wanaostahili kupata matibabu bure. Zoezi linaendelea ikiwa lengo ni kuchapisha vitambulisho 7,500 vya wazee na Taratibu za kuwapatia wazee vitambulisho vyao zinaendelea kupitia watendaji wa kata.

14. Pia, zoezi la uhamasishaji wananchi kujiunga na mfuko wa Afya ya jamii limefanyika. Na wananchi wameendelea kujiunga na mfuko wa afya ya Jamii na fedha zinazopatikana zimeendelea kutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na uborehsaji wa huduma za afya. Wananchi wote wanahamasishwa kujiunga na mfuko wa Afya ya jamii ili kuongeza mapato ya vituo vya huduma za afya ili kuongeza uhakika wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Hivyo, wananchi mnatakiwa kujiunga na mfuko wa huduma kwa jamii (CHF) ili kupunguza gharama za matibabu.

15. Katika kuhakikisha huduma za maji zinasogezwa kwa wananchi na kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu. Ujenzi wa mradi wa Maji ya bomba kwa Mji wa Kaliua unaendelea ambapo jumla ya vituo 20 vya kuchotea maji na pampu house 2 zimejengwa. Pia, jumla ya vituo 6 vya kuchotea maji vimejengwa na pampu house 1 katika kijiji cha kazanaupate. Ulazaji wa bomba (transmission) kwa kutoka chanzo cha maji hadi kwenye tanki kuu umekamilika. Vivyohivyo, ujenzi wa mradi wa maji ya bomba katika vijiji vya Maboha na Mitimitano utaanza muda wowote.

16. Uchimbaji wa visima virefu 4 vijiji vya Ugunga, Imalampaka, Uhindi na Kanoge umefanyika kupitia ufadhiliwa wa kampuni ya JTI. Vivyohivyo, taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu 24 zimekamilika, bado kupata kibali cha kusini mkataba toka Wizara ya maji. Vijiji vitakavyonufaika ni Makingi 1, shella 1, Ukumbisiganga 1, Uyumbu 1, Mwendakulima (Uyowa) 2, Nsungwa 1, Seleli 1, Igwisi 1, Ulindwanoni 1, Ibambo 1, Nhwande 1, Sasu 1, King'wangoko 1, Imalamihayo 1, Limbula 1, Zugimlole 1, Kombe 1, Kanindo 1, Usangi 1, Usimba (Zugimlole), Usimba (Usimba) 1, Usigara 1 na Kagera 1.



Scanned by CamScanner

17. Pia, shughuli za usanifu wa Ujenzi wa bwawa la Ichemba B umekamilika na taarifa ya usanifu imewasilishwa Wizara ya Maji kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa bwawa, ufuatiliaji wa kupata bajeti ya utekelezaji unaendelea kufanyika.
18. Katika jitihada za kuongeza kipato kwa wananchi na kupunguza utegemezi wa zao la tumbaku. Halmashauri imehamasisha kilimo cha mazao ya biashara Pamba, alizeti na korosho. Ili kuhakikisha mbegu za korosho zinapatikana, halmashauri, imenunua mbegu za kutosha na kuzipeleka kwa watendaji wa kata ili kurahisiha upatikanaji wa mbegu hizo karibu na wananchi. Pia, kuwapunguzia usumbufu wananchi kufuata mbegu hizo Wilayani. Mbegu hizo ziliuzwa kilo 1 Tshs 6,000/= ambayo inatosha kupanda ekari 3. Hivyo, niwashukuru wananchi kwa kununua mbegu hizo.
19. Sambamba na hili, Vyama vya ushirika 6 vya pamba vimeanzishwa na taratibu zinaendelea za usajili na maelekezo mengine kwa baadhi ya Vyama. Vyama hivyo ni: Mwembeni Amcos, Utulivu Amcos, Wachawaseme Amcos, Igombe mabadiliko Amcos, Usinge Amcos na Bulela Amcos.
20. Upembuzi yakinifu wa mnada wa mifugo wa Wilaya umefanyika na andiko la mnada limekamilika. Pia, michoro ya mnada na makisio ya gharama za ujenzi wa miundombinu ya mnada huo zimekamilika na kuwasilishwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili taratibu zingine ziendelee.
21. Uandaaji wa ramani na Upimaji wa viwanja jirani na eneo la jengo la hospitali ya Wilaya umefanyika. Jumla ya deed plan 12 za viwanja zimeandaliwa kisha kuwasilisha kwa Mkurugenzi msaidizi wa upimaji na ramani wa kanda ya magharibi kwa ajili ya kuidhinishwa.
22. Utoaji wa mikopo umefanyika kwa vikundi vilivyokidhi vigezo katika kata zote. Jumla ya shs 207,050,000/= zimetolewa kwa mchanganuo ufuatavyo; Sh 101,050,000/= kwa vikundi vya wajasiliamli vijana, Sh96,000,000/= kwa vikundi vya Wanawake na shs 10,000,000/= kwa vikundi vya Walemavu. Hivyo, niombe vikundi vilivyokopeshwa kurejesha marejesho yao kwa wakati ili vikundi vingine viweze kupatiwa mikopo.



Scanned by CamScanner

23. Uhawilishaji wa fedha (TASAF III) Tzs 1,203,024,300.00 kwenda kwa walengwa wanaonufaika na Mpango wa kunusuru Kaya maskini.
24. Halmashauri imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa uzio wa jengo la Halmashauri na ujenzi wa ukumbi wa Halmashauri. Ambapo kwa sasa jengo la ukumbi wa kisasa lipo hatua za ukamilishaji.
25. Ununuzi wa magari mawili toyota Landcruiser (hard top) na Toyota Double caben umefanyika na magari yameshapokelewa. Pia gari jingine (Toyota Double caben) linatarajiwa kununuliwa.

## 2.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAPATO YA NDANI MWAKA 2018/19

**Ndugu Wananchi,**

Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilikisia kukusanya na kutumia mapato kutokana na vyanzo vyake vya ndani yenye jumla ya Tzs. 4,440,067,500.00. Hadi tarehe 30/06/19, jumla ya Sh. 2,897,009,238.82 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 65 ya malengo. Nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshiwa madiwani wote na wataalamu kwa ushirikiano wenu katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Katika utekelezaji na usimamizi wa shughuli za Halmashauri kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Juni, 2019, changamoto kwa ujumla zilizojitokeza ni kama ifuatavyo:-

1. Kuchelewa kwa fedha za miradi kutoka Serikali Kuu na wafadhili hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ngazi ya Vijiji.
2. Upungufu mkubwa wa miundombinu ya kutolea huduma kwa jamii kwa sekta za afya na elimu kama vile Vyumba vya madarasa shule za msingi na sekondari,nyumba za walimu na mabweni,chumba cha upasuaji nk..
3. Uhaba wa magari katika kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli zinazotekelezwa katika ngazi za kata na Vijiji.
4. Upungufu wa Watendaji wa kata na vijiji hali inayosababisha kupunguza ufanisi wa kutekeleza shughuli zinazotekelezwa katika ngazi ya Kata naVijiji.



Scanned by CamScanner

## 2.4 MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

**Ndugu Wananchi,**

Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo:-

1. Halmashauri imeanza ujenzi wa maabara katika Hospitali ya Wilaya. Ufuatiliaji wa usajiri wa zahanati zilizokamilika za Ibambo, Nsimbo, Kasungu na Imalampaka ili ziweze kufunguliwa na kuanza kutoa huduma zilizokusudiwa.
2. Kuendelea kuhamasisha wananchi juu ya ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za jamii kama zahanati,vyumba vya madarasa, vyoo, nyumba za walimu na madawati.
3. Halmashauri itaendelea kuwasiliana na Tume ya menejimenti ya utumishi ili iweze kutupatia watumishi wanaohitajika katika kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi.

## 3.0 HITIMISHO

**Ndugu Wananchi,**

Ukuaji wa Uchumi na maendeleo ya kaliua yanategemea kwa kiasi kikubwa juhudi za Wanakaliua wenyewe. Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Wananchi hususani katika sekta za umeme, Afya, Elimu,barabara nk.

Nichukuc fursa hii kuwaom
ba Wananchi wa Kata zote za Kaliua kushiriki kikamilifu katika kukabiliana na changamoto zinazo-tuzunguka. Aidha, tutumie kikamilifu fursa zinazopatikana ili kuweza kujiletea maendeleo sisi wenyewe na Taifa kwa ujumla.

***Mungu Ibariki Afrika, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu ibariki Kaliua***



Scanned by CamScanner